

# **HISTORIA YA WANYIRAMBA, UTAMADUNI NA VIVUTIO VYA IRAMBA**



**KITTO.J.I.B**



## **Dibaji**

Taifa lolote lisilo na utamaduni ni sawa na taifa lililokufa ,Wanyiramba na watanzania kwa ujumla wanajivunia amani,utulivu,umoja na mshikamano tulionao ni kwa sababu unatokana na utamaduni tulioijijengea. Nguzo za utamaduni huu ni pamoja na mila na desturi zetu,lugha , sanaa, michezo, utunzaji wa mazingira, vielelezo vyta utamaduni na historia yetu.Hata hivyo,utamaduni wa Wanyiramba unafifia polepole ni kutokana na kutokuzingatiwa kikamilifu . Nafurahi kwamba kitabu hiki kitatoa upeo na ufahamu kwa jamii juu ya utalii wa kiutamaduni, mila na desturi, lugha, sanaa, michezo na rasilimali zilizomo Wilayani Iramba. Ufanisi katika utekelezaji wa maudhui ya kitabu hiki utategemea sana ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi, mashirika na wananchi kwa ujumla pia kimezingatia mawazo, michango maoni na mapendeleko kutoka kwa wazee, watu binafsi, viongozi wa dini siasa na wataalam wa fani za utamaduni.

Ninayo imani kubwa kwamba wananchi watapata fursa ya kukisoma kitabu hiki na kukielewa vizuri ili kushiriki kikamilifu katika kuulinda, kuutunza na kuutangaza utamaduni wa wanyiramba na maeneo ya utalii wa kiutamaduni.

JOHN I.B.KITTO  
0784 761871

AFISA UTAMADUNI (W)

**IRAMBA.**

## **Shukrani**

Napenda kuwashuru wote walioshiriki kuchangia mawazo yao katika kazi hii.

Baadhi ya hao ni; Mzee N. Nkurulu, Mchungaji Mdinda, Mzee Urembo(marehemu), Mzee D. Mkoma, W. Gelege,Mzee Kitto, Mzee Ntintii, Mzee Shankunkuli, Mzee Raphael A. Mkumbo (Mzee Mnyiramba), Mzee C. Mkumbo, Mzee J. Mliga na wazee wengine wengi ambao sijawataja majina yao natambua mchango wao Mungu awabariki sana.

Kipekee namshukuru sana Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri Ya Wilaya ya Iramba Ndugu, L. P. Mwageni kwa ushirikiano wake.

Aidha Nawashukuru Ndugu Dandala, M (Aliyekuwa Afisa Tawala Wilaya ya Iramba) na Ndugu Emmanuel A.Migunga kwa ushauri na maelekezo yao.

## **Lengo la Kitabu Hiki Kiutamaduni.**

Kukuza, Kudumisha na Kuhifadhi urithi wa asili na Utamaduni wa Wanyiramba.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa lengo hilo, Serikali ichukue hatua zinazofaa ili: -

- (a) Kulinda na kuhifadhi Urithi wa asili, Malikale na sehemu zenyе umuhimu wa kihistoria ili kuepuka uharibifu, wizi au utoroshaji nje ya nchi.
- (b) Kulinda, kuhifadhi na kuendeleza Utamaduni wa Wanyiramba na Jamii nyingine zilizomo Iramba.
- (c) Kujenga utamaduni wa kuwepo ushirikiano, maelewano, maridhiano, uvumilivu na kuheshimu Mila, Desturi na imani ya Dini ya kila mtu.
- (d) Serikali kuingiza Wilaya ya Iramba kwenye ramani ya Dunia juu ya mambo ya kale, iweze kuingizwa kwenye vitabu vyta kihistoria na jumba la makumbusho.

## **Dira**

Kuhakikisha kunakuwepo na uhifahi endelevu wa Utamaduni, Mila na Desturi, Rasilimali na Utalii bila kusahau mazingira kwa Ustawi wa Maisha, Uchumi, Maendleo na Utawala bora kwa Jamii ya Iramba na Taifa kwa ujumla

## **Mtazamo**

Kuhifadhi, kutangaza na kuboresha Utamaduni, Mila na Desturi, Rasilimali na Utalii kwa ajili ya Ustawi wa Jamii ya Wanyiramba na Taifa kwa ujumla kwa kuzingatia yafuatayo:-

- (i) Kuandaa mkakati na taratibu sahihi zinazostahili kuhifadhi Utamaduni, Rasilimali na Utalii wa Iramba.
- (ii) Kuweka sheria ndogo ndogo na kanuni za kuhifadhi Utamaduni, Rasilimali na Utalii wa Iramba .
- (iii) Kusimamia na kutathmini utekelezaji wa mikakati iliyowekwa ili:

- (a) Kuhakikisha mipango yote inatekelezwa kwa kufuata mikakati na taratibu zinazostahili
- (b) Kuhakikisha mfumo wa sheria ndogo ndogo za utamaduni, mila na dsturi, Rasilimai na Utalii zilizomo katika maeneo husika uko wazi na unatekelezeka.
- (c) Kufikia kiwango cha juu cha ulinzi wa Utamaduni, Mila kale, Rasilimali na Utalii.
- (d) Kuchukua hatua stahii za kutangaza ana kupanua wigo wa shughuli za Utamaduni na Utalii katika Wilaya ya Iramba.
- (e) Kuendeleza uwezo wa kitaaluma kwa Vijana na Jamii kwa ujumla lengo ni kuibua, Kufuatilia, Kutambua na kuboresha Utamaduni, Mila na Desturi, Rasilimali na Utalii, Urithi wao.

### **Matarajio**

Baada ya Jamii mbalimbali kukisoma Kitabu hiki natarajia mambo yafuatayo: -

- (i) Ni Jamii kuwa na ari ya kuandika Vitabu na makala mbalimbali zitakazoelezea Utamaduni, Mila na Desturi, Mali kale, Rasilimali na Utalii wa Iramba kwa faida yao na Taifa kwa ujumla.
- (ii) Jamii na Wadau walioko ndani na nje ya Wilaya ya Iramba kuchangia kwa hali na mali michango yao ili kujenga Kituo/Nyumba ya makumbusho kwa ajili ya kuhifadhi Mali kale, Utalii wa Kiutamaduni, Mila na Desturi za Iramba. Kituo hicho kitajulikana kwa jina la **IRAMBA RESERVE CULTURAL CETRE (IRECUCE)** ambapo Makao yake Makuu yatakuwa Mjini Kiomboi.
- (iii) Vijana na Jamii kwa ujumla watahamasika na hivyo watakuwa tayari kuibua, kutambua, kuendeleza, kuboresha na kulinda Utalii wa Kiutamaduni, Mila na Desturi na Rasilimali zake zilizopo Iramba.
- (iv) Jamii itakuwa imepata uelewa kuhusu Udamaduni, Mali kale, Mila na Desturi na Rasilimali zilizomo katika mazingira yake na Iramba kwa ujumla. Kwa kufanya hivyo, Jamii itawenza kuhifadhi, kuthamini, kupenda, kulinda na hatimaye kuendeleza kama sehemu ya urithi wa sasa na baadaye.


# **YALIYOMO**

Lengo la Kitabu Hiki Kiutamaduni.....	iv
Dira.....	iv
Mtazamo .....	iv
Matarajio .....	v
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI.....	1
SURA YA PILI .....	2
Historia Ya Wanyiramba.....	2
Uhusiano kati ya Wanyiramba na Wanyisanzu.....	4
SURA YA TATU .....	5
Koo Za Kinyiramba.....	5
SURA YA NNE .....	8
Kinyiramba asili yake ni Kibantu.....	8
1.     Tungo (Sentensi) Za Kinyiramba.....	8
2.     Vitenzi vya Kinyiramba na Kibantu .....	8
SURA YA TANO .....	11
Kuanzishwa Kwa Wilaya ya Iramba .....	11
SURA YA SITA.....	16
Maeneo yenze Vivutio vya Utalii wa Kiutamaduni .....	16
Utamaduni .....	26
Mila na Desturi.....	26
Utani Bainya ya Koo na Koo, Wanyiramba na makabila mengine.....	27
Ndoa .....	27
SURA YA SABA.....	31
Tarafa, Kata na Vijiji vya Wilaya ya Iramba .....	31

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Wilaya ya Iramba ipo kati ya latitudo  $4^{\circ}$ ,  $3^{\circ}$  Kusini na Longitudo  $34^{\circ}$  na  $35^{\circ}$  Mashariki upande wa Kaskazini ina pakana na Wilaya ya Meatu, upande wa Mashariki imepakana na Wilaya ya Mkalama, Upande wa Kusini imepakana na Wilaya ya Singida, Upande wa Magharibi imepakana na Wilaya ya Igunga na Upande wa Kaskazini imepakana na Wilaya za Maswa na Meatu.



## **SURA YA PILI**

### **Historia Ya Wanyiramba**

Kabla ya Wakoloni kuingia barani Afrika, Makundi mbalimbali jamii ya wabantu walisafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine aidha kutafuta makazi salama au kufanya shughuli zingine za kibinadamu.

Wanyiramba walikuwa mionganini ya jamii iliyosafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na hatimaye kufika walipo sasa. Inasemekana Wanyiramba walitokea Sudani. Walianza safari yao wakielekea Kusini mwa Afrika hadi walipofika Pwani mwa Kenya (Mombasa) ambapo waliweka makazi yao hapo, Shughuli yao kubwa ilikuwa ni kilimo na uvuvi wa Samaki.

Jamii hii iliongezeka kiasi cha kuanza kugombea ardhi na jamii nyingine. Kundi kubwa liliondoka na kuelekea Kusini Magharibi mwa Kenya ambapo walijikuta wamefika Kandokando mwa ziwa Nyanza (kwa sasa Victoria) Mkoa wa Mara (Musoma). Hapo waliwakuta wenyeji wao yaani Wakurya, Wajita, Wakerewe nk. Wanyiramba waliishi hapo na kuanza kuongezeka, wenyeji wao walipoona idadi ya watu inaongezeka, wakahofia kunyang'anywa ardhi yao. Ndipo walipotaka kuanzisha vita baina yao na wageni. Wakiwa kwenye eneo la mapambano, kwa mshangao mkubwa pande zote mbili zilishuhudia radi ikipiga kwa nguvu katikati yao na hali kipindi hicho hakikuwa cha mvua. Baada ya kuona hivyo jamii hizo ziliachana na fikra ya mapigano.

Jamii hizi zilikaa na kutafakari, "kwa nini radi ilipiga hali haikuwa kipindi cha mvua?", Viongozi wa Kinyiramba na Kikurya walifikiri sana kutokea kwa radi hiyo. Hivyo walishikana mikono na kusema, "sisi tumekuwa ndugu, hivyo hakuna sababu yoyote ya kugombana". Wakakubaliana upande mmoja wakae wanyiramba na upande wa pili wakae wenyeji. Maisha yaliendelea kwa pande zote, hata hivyo viongozi wa kimila wa kinyiramba walitafakari na kufikiri sana, wakaamua kuwaeleza wenyeji wao kwamba "Sisi na ninyi tumekuwa ndugu hivyo hakuna sababu ya kugombea ardhi , tuachenii tuondoke tukatafute eneo jingine la

kuishi". Kundi kubwa liliondoka Musoma na baadhi walibaki hapo na kujichanganya na makabali mengine. Kundi hilo lilielekea Kusini Mashariki mwa Ziwa Nyanza kwa sasa victoria na kujikuta wamefika Milima ya Usambara, wakamua kuishi hapo kwa muda, baada ya hapo waliondoka hadi walipofika eneo la Upareni nako hawakukaa sana bali waliondoka na kuendelea na safari yao hadi walipofika Morogoro, hapo waliishi kwa muda kwani waliamua kuondoka kuendelea na safari yao. Hata hivyo huko nyuma baadhi ya wanyiramba walibaki kuendelea na maisha, ushahidi wa kihistoria na wakisayansi unajitokeza pale majina yenye asili ya kinyiramba kuwepo katika maeneo yote waliopita kwa mfano, Makala, Msensi (msangi), Sha-mwelu (She-muhilu), Kitundu, mbogo nk. Baada ya hapo walielekea Iringa, huko waliwakuta wenyeji wao wakarimu sana walikaribishwa lakini wakaelezwa, kwamba ardhi yote imemilikiwa na wenyeji tena iko chini ya utawali wa kimila. Hivyo waliondoka kuelekea Kaskazini Magharibi mwa Iringa hadi walipotokezea Itigi Mkoani Singida huko waliwakuta Wabarabaig wakijishughulisha na ufügaji wa ng'ombe. Wanyiramba na Wabarabaig walikubaliana kubadilishana mali walizokuwa nazo. Wanyiramba waliwapatia Wabarabaig Mapambo waliyoyapata baharini na Mbegu walizozibeba na Wabarabaigi waliwapatia wanyiramba mifugo. Wanyiramba hawakupendezwa sana kuishi hapo hivyo waliamua kuondoka na kuendelea na safari yao. Katika kuondoka kwao makundi mawili yaligawanyika jingine lilipita mwambao mwa Tabora na hatimaye kufika sehemu iitwayo Lunua (Ushora – Ndago).

Kundi jingine likaelekea Kaskazini ambapo walikutana na Wanyaturu. Wanyaturu hawakutaka kuwaruhusu wanyiramba kupita hapo,kwa kuwa wanyiramba hawakuwa na nia ya kuishi hapo, waliamua kupambana na wanyaturu kwa mapigano makali.Baada ya kufanikiwa kupita waliendelea na safari kundi dogo liliachwa eneo la Kirumi likaendelea na maisha yao, kundi kubwa lilisonga mbele hadi lilipofika eneo la Kisiriri. Hapo walivutiwa na eneo hilo wakaamua kuweka makazi yao . Kadri walivyoongezeka waliendelea kutawanyika na kwenda sehemu mbalimbali kama vile:- Nduguti, Gumanga, Kinampanda, Ulemo, Iambi, mkalama, Ibaga, kinyangiri na wengine walishuka Shelui(bonde la ufa) wakakutana na wale wa ndago ambapo na wao waliendelea kutawanyika

maeneo mbalimbali ya Iramba. Kutokana na mtawanyiko huo lugha ya kinyiramba ilianza kutofautiana kidogo ***kilahaja***. Maana ya lahaja ni tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika lugha yenye asili moja.

### **Uhusiano kati ya Wanyiramba na Wanyisanzu**

Inasemekana kuna unasaba mkubwa kati ya wanyiramba na wanyisanzu, hii inatokana na ushahidi wa kihistoria na kisayansi kama ifuatavyo;

Wanyiramba na Wanyisanzu mila na desturi, sanaa na utamaduni hazitofautiani kwani ni zile zile. Kwa mfano:- Majina ya Ukoo (Nduuli) wanyiramba na wanyisanzu hutumika yaleyale kwa mfano, Mpanda (Wanaume) Tyale (Wanawake), Gyunda (Wanaume) Mwani (wanawake), Mpinga (Wanaume) Kyoga (Wanawake) n.k. Aidha Nyimbo zote zinazoimbwa kwenye ngoma na Burudani huimbwa kwa lugha ya Kinyiramba iwe kwa Wanyiramba ama Wanyisanzu.

Ushahidi mwingine ni mfanano na mpangilio wa sentensi na vitenzi kuishia na irabu **a**.

Kwa mfano,

(Kiswahili): *Juma anapiga mpira vizuri.*

(Kinyiramba): *Juma ukua mumpila izaa.*

(Kinyisanzu): *Juma ukua mumpila uzaa.*

(Kinyaturu): *Juma ukua mumpila ijaa*

Kwa ujumla Wanyiramba na Wanyisanzu si watani bali ni ndugu, lakini myiramba ni mtani wa Makabila yote ya Musoma wakiongozwa na Wakurya. Watani wengine wa Wanyiramba ni Wanyaturu. Utani wa Mnyaturu na Myiramba ulikuja hasa pale njaa kali ilipoingia turu kiasi cha kupelekea wanyaturu kuhemea chakula kwa Wanyiramba.

# SURA YA TATU

## **Koo Za Kinyiramba**

Wanyiramba wamegawanyika katika Koo ( Nduli) zaidi ya ishirini Koo hizi zimebainisha Mashina, Majina ya ukoo kwa upande wa Wanaume na Wanawake pia eneo lao la asili. Ukoo mkubwa katika kabilia la Wanyiramba ni “Anambwa” Ukoo huu una matawi (Milongo) zaidi ya sita. Koo zingine ni “Anishung’u, Anambala, Anikyili, Anampanda, Anankumbi, Ananzoka, Anangili, Analilya, Anangu, Aniyuga, Anambeu, Anishanga, Anakumi, Anankamba, Anankali, Asambaa, Anakilima, Azigo, Anawendo na Anilimu.

Ufuatao ni ufanuzi wa koo (nduli za Kinilyamba) kama jedwali linavyoonesha hapa chini: -

NA	KOO	JINSI		ASILI (ENEKO)	UHUSIANISHO
		ME	KE		
1	ANAMBWA (a) Anasitwa	Kiula	Mgalu	- Kisiriri - Ndago - Shelui - Ulemo na - Tutu n.k.	Mbwa Mwekundu
	(b) Anansimba	Makala	Kyunyu	- Kisiriri	Mbwa Mweusi
	(c) Anamkato	Makala	Kyunyu	- Kisiriri	Mbwa mweupe asiyen doa
	(d) Anansungui	Makala	Kyunyu	- Kisiriri	
	(e) Ani-tyaa	Kilimba	Kyunyu	- Kimpunda - Tyaa	Mbwa aliyejikuja mkia
	(f) Analunsanga	Kitila	Kyunyu	- Lunsanga	Mbwa mwenye mabaka
2	ANISHUNGU	Mkumbo Mkumbo	Kilie Mwigoo	-kisharita -munkonze -Galangala	Upopo
3	ANAMBALA	i) Gyole ii) Lyanga iii) Shani	Gyole Gyole Gyole	- Kinambala - Kisiriri	-korongo(ndege) Kinyiramba(mpuugii)
4	ANIKYELI	Msengi	Kyeli	- Kiomboi - Meli na - Ntwike	Simba
5	ANAMPANDA	- Mpanda - Shole	Tyale Tyale	- Kinampanda	-punda nyuki

6	ANANKUMBI	Mgelwa	Mpuzi	- Shelui, - Wembere na - Mkalama	-majani ya maboga -sungura
7	ANANZOKA	i) Mbogo ii) Shukia	Muuza Muuza	-Kisiriri (Tyumba) - Gumanga	Nyati
8	ANANGILI	Shila	Mwile	- Kinyangiri, - - Kisiriri, - Kimagwe	Ngiri
9	ANALILYA	i) Shalua ii) Nsunza iii) Shalua	Mwelu Mwelu Sagi	- Kinalilya	Kanga – Ndege
10	ANANGU/ANA MILAMBO	i) Nkana ii) Nangu	Mbula Nonge	- Shelui - Ntwike - Mingela	-Ngurumo za mvua -Mvua
11	ANIYUGA	Shango	Ntoma	- Kimpunda - NKango	Fisi
12	ANAMBEU	Kingu	Nzitu	- Kinambeu - Mampanta	- Kondoo - Paka
13	ANISHANGA	Mkoma	Nsumbu	- Tulya - Migilango - Kisiriri	- Nyani - Kuku
14	ANAKUMI	Kitundu	Msua	- Kinakumi	Mchwa
15	ANA – NKAMBA	Shumbi	Ntulu	- Msingi - Nduguti	- Chachu (me) - Pombe (ke)
16	ANA – NKALI	Gunda Mpinga Pyuza	Mwani Kyoga Mianzi	- Iambi - Mkalama -Isanzu	- Chui (me) - Jua
17	ASAMBAA	Mgana	Mwingo	- Mkalama - Iambi -Isanzu	-upepo(nzega)
18	ANA – KIZIGO	Yindi	Jima	- Gumanga - Iambi - Mkalama	-Ngombe -Maziwa(mtindi)
19	ANA – MWENDO	Mwendo	Kilima	-Iambi -Mkalama -kinakumi	-mchwa
20	ANI – LIMU	Gwila	Sungi	-Gumanga -mkalama	

Kumbuka kwamba, baadhi ya koo zimetokana na koo zingine(matawi) kama ifuatavyo; ukoo wa *anakizigo* ni tawi la *analilya*, ukoo wa *anamwendo* ni tawi la *anakumi* na ukoo wa *asambaa* umetokana na ukoo wa *anishungu*. Wanaume(akina baba) na wanawake(akina mama) kwa heshima huitwa kwa mjina ya baba zao au watoto wao kwa kuanza na *sha/shi* (kwa wanaume) na *na/ni* (kwa wanawake).

Kwa mfano; *sha-makala*, *shi-shila*, *sha-kiula*, *sha-mkumbo*, *sha-mwile nk*,  
kwa wanawake *huitwa*, *na-mgalu*, *na-kitundu*, *ni-lyanga nk*.

# **SURA YA NNE**

## **Kinyiramba asili yake ni Kibantu**

Lugha ya kinyiramba asili yake ni Kibantu.

Ushahidi wa Kisimu ni ushahidi unaothibitishwa kwa misingi inayohusu Sayansi ya Lugha.

### **1. Tungo (Sentensi) Za Kinyiramba**

Miundo ya tungo (sentensi) za maneno ya Kinyiramba zinafanana sana na miundo ya tungo za maneno ya Kibantu. Kwani sentensi za Kinyiramba na lugha za Kibantu zina kiima na kiarifu.

**K                    A**

Mfano:      Kinyiramba - Baba / Ulyea Ugali  
                  Kiswahili - Baba / anakula ugali

### **2. Vitenzi vya Kinyiramba na Kibantu**

Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya vitenzi vya Kinyiramba na vile vya Kibantu

#### **(a) Viambishi**

Lugha ya Kinyiramba na lugha za kibantu vitenzi vyake hujengwa na mzizi (kiini) pamoja na Viambishi vyake (awali na tamati)

Mfano :-

Kinyiramba - u - Lim - a

Kiswahili - a -na- lim-a

- **Lim** – ni mzizi / kiini

- **A** – kiambishi tamati

#### **(b) Mnyambuliko wa kitenzi**

Mnyambuliko wa vitenzi vya kinyiramba hufanana na ule wa vitenzi vya lugha ya kibantu.

Mfano: Kinyiramba - Kusheka - Kushekesh - Kushekolela

**(c) Mwanzo wa Vitenzi**

Vitenzi vyote vya Kinyiramba na vile vya lugha za Kibantu huanza na viambishi viwakilishi nafsi.

Mfano:	Kinyiramba	-	Nigenda	-	Nalongola
	Kiswahili	-	Ninatembea	-	Nakwenda

Kiambishi **Ni, Na** ni viambishi viwakilishi nafsi.

**(d) Mwishilizo wa vitenzi**

Vitenzi vya lugha za Kibantu na Kiswahili huishia na Irambu – **a**

Mfano:	Kinyiramba	-	Kukisiga	Kua	Manka
	Kiswahili	-	Kucheza	Piga	Kimbia

Lugha ya Kinyiramba hutumia lugha ya picha ambao huwa ya ukweli na maana ya ufigo sana ambapo huweza kufisha ujumbe kwa jamii ili kujifunza. Mfano, Semi za Kinyiramba: -

<b>NA</b>	<b>KINYIRAMBA</b>	<b>KISWAHILI</b>	<b>KIUNGEREZA</b>
1	Mwili kisonga Mukola	Mwili hutunzwa na mwenyewe	The body is kept by owne
2	Inkamilo zikilonda	Undugu ni Kushirikiana	Fraternity/Brotherhood is cooperation
3	Intondo imalunde	Ipo siku moja	One day yes
4	Nishunta intondo lukapinda	Nasogeza siku kadri Mungu anavyonijalia	I buy a day by providence
5	Nukuduma ukuligagya	Atafutaye hupata	Edurenth is promising
6	Umwananusimbe iliso pansi	Mwanamaskini jicho lake daima chini	The destitute won't be tired to loot for, its eyes always down
7	Ushunta sika ukinuna	Mganga hajigangi	The physician won't medicate oneself
8	Tyuti nu Maluka	Rafiki pete na Kidole	The friend with close intimacy
9	Intiti zaiyenga Mipama	Watu kurejea maskani nyakati za jioni	Birds retneat to their nests
10	Umukaku ukugula	Asiyesikila la	The one who is

	ituwe	Mkuu huvujika guu	obstinate will suffer for the consequences
11	Ukakumsinga zangu	Kufanya usichokiweza	Scrutching a cat
12	Inshoke ngila kaulime	Katika msafara wa maisha hakuna kurudi nyuma	Retreat no surrender
13	Kitengani kina masala ni kitegwa kina masala	Fumbo mfumbie mjinga mjanja atalig'amua	Riddle for an ignorant person but for the craftman will disclose.

Misemo mingine ya kinyiramba ni:-

- Impinda ya Mwanangulu umalile umukenki  
Tafsiri yakeni: - Uzito wa mzinto anafahamu mbebaji
- Msekwa washokile ni Ng'ombe  
Tafsiri yake ni mtu aliyedhadhauliwa alirudi na mifugo. Maana yake  
usimdharaau mtu huji kesho atapata nini
- Musuli wa Mbwa ukukopangwa kinakili upiu  
Tafsiri yake ni Mchuzi wa Mbwa hunywewa ungali wa moto,  
maana yake ni vema kuchukua tahadhari mapema kabla  
halijaharibika jambo  
Muuzaa ukulegagwa nulekelwa

### **Vitendawili vya Kinyiramba**

- Fanani: Laale laale - Kitendawili  
 Hadhira: Laale - Tega  
 Fanani: Mweli Mukyeko - Mwezi katika kipeyu  
 Hadhira: Masunsu - Maziwa  
 Fanani: Kiite Muntunda - Uweusi Mtunguni  
 Hadhira: Ndalu - Mlenda uliokaushwa

# **SURA YA TANO**

## **Kuanzishwa Kwa Wilaya ya Iramba**

Wilaya ya Iramba ilianzishwa mwaka 1954,awali makao makuu ya wilaya ya Iramba yalipelekwa kijiji cha Mkalama,huko hayakudumu Kwani yalihamishiwa katika kijiji cha kisiriri,hata hivyo watawala walipendezwa zaidi na eneo Kiomboi ambalo lilikuwa na miti mingi aina ya miombo kwa kinyiramba huitwa “**mupumpu**”.Wazungu walishindwa kutamka neno miombo na badala yake wakawa wanatamka **kiomboi**,neno hili lilipata mashiko kwa watumiaji kiasi cha kukomaa na kuwa **Kiomboi**, wilaya ya Iramba imeongozwa na wakuu wa wilaya mbalimbali kama ifuatavyo;—

- 1.** Dunstan A.Omari- 1958-Juni 1959,
- 2.** Athuman Katuo -Julai 1959-Novemba 1960,
- 3.** John M.Ndingwangu- Des. 1960-Juni 1961,
- 4.** Samwel A.Msindai- Julai 1961- Nov 1962,
- 5.** Sumbu Gallawa- Des.1962-Jan.1963,
- 6.** G.M.Bundalla Feb.1963-Mei.1966,
- 7.** G.O.Mhagama - Juni.1966-Machi,1967,
- 8.** A.K.Msonge        A pril.1967-Des.1971,
- 9.** M.B.Kig'ombe Jan.1972-April 1977,
- 10.** R.S.Chazua Julai 1977-Juni.1983,
- 11.** Jeremia E.Duve Julai 1983-Mei 1986,
- 12.** A.K.Mwakyusa Mei 1986-Nov.1990,
- 13.** E.M.Halinga Des.1990-Mei 1992,
- 14.** John Z.Chiligati- Juni 1992-Des.1996,
- 15.** David W.Hollela- Jani 1997-Aprili 1998,
- 16.** Zainabu M.Kondo Aprili 1998-Agosti 2006,
- 17.** Grace H.Mesaki Agosti 2006-Mei 2012,
- 18.** Yahya E.Nawanda Mei 2012-Machi 2015,
- 19.** Lucy Mayenga Machi.2015-Julai 2016,
- 20.** Emmanuel J.Luhahula Julai.2016-



Jengo la Mkuu wa Wilaya ya Iramba

### **Kuanzishwa Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba**

Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilianzishwa mwaka 1984, Wakurugenzi watendaji wa halmashauri ya wilaya walioongoza wilaya hii ni hawa wafuatao;

1. George Challe-1984-1985,
2. Masanga B.Msonge-1985-1988,
3. Kabeja B.Moses-1988-1990,
4. Fredrick kipigapasi-1990-1995,
5. Berther Swai-1995-1997,
6. Mr.Msoma-1997-1998,
7. Ester Mbigili-1998-2000,
8. Mpangalukela Tataala-2000-2004,
9. Dr.Izidor Mtalo-2004-2007,
10. Fortunatus Fwema-2007-2012,
11. Christine K.Midello-2012-2013,

12. Halima Mpita-2013-2015,
13. Dr. Grace Mbaruku-2015-2015,
14. Clement Berege-2015-2016,
15. Linno P. Mwageni-2016-



Jengo la halmashauri ya wilaya ya Iramba.

### **Siasa**

Wilaya ya Iramba imeweza kushiriki kikamilifu katika masuala ya siasa, hii ni pamoja na kufanya chaguzi mbalimbali kuwapata viongozi kuanzia ngazi ya shina hadi taifa

1958-1965 – Samwel Msindai

1965-1970 – Yona J. Nkurlu

1970-1975 Jimbo la Iramba liligawanywa majimbo mawili yaani Iramba ya juu na Iramba ya chini, ambapo Iramba ya juu alichaguliwa.

Mchungaji Simion P. Kinzu na Iramba ya chini alichaguliwa Ndg Abel Nalizingwa.

1975-1980- Likarudishwa jimbo moja la Iramba lililoongozwa na Nassania Y. Nkurlu

1980-1995- Alichaguliwa Mhe, Nalaila L. Kiula

1995- Jimbo la Iramba liligawanywa majimbo mawili, jimbo la Iramba Magharibi na Iramba Mashariki, Nalaila Kiula aliongoza jumbo la Iramba magharibi na Mgana Msindai aliongoza Iramba Mashariki.

1995-2000- Nalaila Kiula (Iramba Magharibi).

2000-2005- Leonard Shango (Iramba Magharibi)

2005-2010- Juma Kilimba (Iramba Magharibi)

2010-2015- Mwigulu L. Nchemba (Iramba Magharibi)

2015- Dr. Mwigulu Lameck Nchemba

Mhe Diana Mkumbo Chilolo na Martha Mlata ni wabunge waliochaguliwa kupidia viti maalumu wanawake kwa tikit ya CCM Mkoa wa Singida.



Mzee Nassania Nkurlu aliyewahi kuwa mbunge wa Iramba mwaka 1975-1980.

## **Mwenge wa Uhuru**

Wilaya ya Iramba haitasahau na kusahulika katika historia ya Tanzania Pale ilipo pewa heshima ya kuzindua mbio za mwenge wa uhuru kitaifa kwa kuwashaa mwenge wa uhuru tarehe 01/08/ 1997, mgeni rasmi siku ya uzinduzi alikua Mhe, Waziri kiongozi wa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar Dr.Mohamed Gharib Bilal.Sherehe hizo zilifanyika katika kiwanja cha minyaani(kwa sasa mabatini) mjini Kiomboi.



Mnara huu ulijengwa mwaka 1997 kwa kumbukumbu ya kuzinduliwa mbio za mwenge wa uhuru kitaifa mjini kiomboi wilayani Iramba.

## **SURA YA SITA**

### **Maeneo yenye Vivutio vya Utalii wa Kiutamaduni**

Yafuatayo ni baadhi tu ya maeneo yenye vivutio vya utalii wa utamaduni Wilayani Iramba.

### **Kisana Kwa Mang'ombe**

Eneo hili lipo kijiji cha Kisana, Kata ya Kisiriri, Tarafa ya Kisiriri, kuna michoro ya Wanyama kwenye miamba ya mawe, wanyama hao ni ng'ombe na mbuzi.



Mchoro wa mnyama uliochorwa kwenye mwamba wa jiwe.

### **Ruruma**

Ni Kijiji maarufu katika histori ya Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida na Tanzania kwa ujumla hususani suala la kuanza kwa Injili.

Wamisionari kutoka Ujerumani Bw. Itanai na Bw. Everest walifika **Ruruma Desemba 24,1911** kwa lengo la kujenga Kanisa na kueneza Injili. Baadhi ya Wazee waliokutana na Wamisionari hao ni Ndg. Lyanga Munkyala, Ndg. Mkumbo Kilili na Ndg. Nsimpule Kishei.

## Mti wa Kubatizia

Huu ni maarufu katika Kijiji cha Ruruma, Wilaya ya Iramba Dayosisi ya Kati, kwani mwaka **1914** Waumini walibatiziwa mahali hapo kwani hapakuwa na Kanisa miti huo kwa Kinyiramba huitwa “**mutuilankolo**”.



Huu mti (**mutuilankolo**) ulitumiwa kama eneo la kuabudia waumini wa kikristo upo katika kijiji cha Ruruma.

Baadhi ya Waumini waliobatizwa ni Ndg. Yakobo Ntundu, Ndg. Yesaya Mpondo, Ndg. Stephano Magia, Ndg. Mukolamulamu Kidedema na Ndg. Mathayo Gongia.

Mwaka **1933** Waumini wa Kinyiramba walianza kubatizwa kwa majina ya Kikristo lakini yenye asili ya Kinyiramba, kwa mfano majina ya wanaume: Nalompa, Nalogwa, Nagunwa, Napangata, Naukigwa, Nasoloa, Nashokigwa, Nakamia, Nakembetwa, Nalingigwa, Najulwa, Nakomolwa, Nalindilwa, Nalumba, Nalumbikya, Nagomolwa, Naliglia, Niitwa, Nasania, Nasagulwa, Napunigwa, Nasunzwa, Nasupya n.k.

Kwa upande wa Wanawake ni: - Wansokya, Wasangula, Wankembeta, Wampumbulya, Wanindila, Wantwala, Wanguna, Wanduta, Wamilika, Wankolela, Wankumbasa, Wandegya, Wanonda, Wansugumilya, Wansugamilya, Wandaila, Wanimikya, Wantongela, Wangomola, Wantunguila, Wantungata, Wanzalilya, Wampela, Wamona, Wanduta,

Welu, Wampapa, Wandishya, Wampunya, Elinkaila, Eliwaza, Eliwanzita, Winjuka, Wintyapa, Elintongela, Msalawelu, Ulumbi, Lumbikya, Wanumbilya, Ukende, Wanumbikya, Wanansula, Wansola, Tyatawelu, Wingwila, Wampandila, Wanzesya, Wampeta, Wansolania, Wanompela, Wanzita n.k.

### **Kisana Wanguu**

Eneo hili lipo kijiji cha kisana, Kata ya Kisiriri, Tarafa ya Kisiriri kuna mchoro ya mnyama (tembo) kwenye mwamba vile vile kuna eneo la kufanyia matambiko (ibada za asili) kwa Kinyiramba huitwa “kupolya”, eneo la kutambikia huitwa “tyekelo”. Vile vile kuna pango lenye ngoma zilizotumiwa na watu wa zamani.



Ngoma za asili zilizohifadhiwa ndani ya pango –  
zilitumiwanawatuwazamamnikwaajili ya matambiko – eneo la Kiasana

## **Kisharita**

Eneo hili lipo kijiji cha Kisharita, Kata ya Kinampanda Tarafa ya Kinampanda, hapa kuna jiwe mithili ya Kiti ambacho kilikuwa kinakaliwa na kiongozi wa jadi (Mtemi mdogo) Shuluwa. Alifanya miujiza minge ya kustaaajaabisha kiasi cha kuwafanya adui zake (Wajerumani) kushindwa kumkamata ili wamuue. Mtemi shuluwa alijisalimisha kwa Wajerumani na kupelekwa kilimatinde Manyoni Mkao wa Singida hatimaye kunyongwa. Fuvu la Mtemi huyu lipo Ujerumani hadi leo, Jitihada ya kurudisha fuvu hilo Wilayani Iramba bado hazijafanyika.



Jiwe hili lililochongwa mithili ya kiti lilikaliwa na kiongozi wa jadi Shuluwa lipo katika kijiji cha kisharita.

## **Ziwa Kitangiri na Bonde la Wembere**

Ziwa hii limepita katika Tarafa za Shelui na Kisiriri wilayani Iramba. Shughuli zifanywazo katika ziwa hili ni uvuvi wa samaki wa aina mbalimbali kama vile; Kambare, Kamongo, perege, nembe na ningu. Kuna Wanyama waishio humo kama vile kiboko nk. Pia kuna ndege wengi wa aina mbalimbali wazuri wa kuvutia ndege hao ni; flamingo, korongo, ndegemwambu (bwana usafi), fongafonga, batamaji, batamzinga n.k. Aidha pembezoni mwa ziwa hili kuna bonde la wembere mlima

Sekenke-Tulya ambapo inasadikika kuwepo kwa rasilimali nyingi ikiwemo mafuta na madini ya aina mbalimbali.



Ziwa kitangiri limekuwa chanzo kikubwa cha uchumi katika wilaya ya Iramba kwa kutoa aina mbalimbali za samaki.

### **Nkokilangi**

Eneo hili lipo kijiji cha Nkokilangi Kata ya Ntwike, Tarafa ya Shelui, Ni eneo maarufu kwa utengenezaji wa chumvi kwa njia ya kienyeji.Pia eneo hili lilitawaliwa na mtemi Kilyoma alikuwa na miujiza mbalimbali kama kutoweka mikononi mwa maadui zake bila wao kujua amepotelea wapi .Kilyoma alinyongwa na wajerumani eneo la Ntwike,Tarafa ya shelui,Wilaya ya Iramba,kichwa chake kilipelekwa Ujerumani hadi leo bado kipo huko.



Eneo hili ndilo linalosadikika aliponyongewa kiongozi wa jadi Kilyoma.



Usindikaji wa chumvi Nkonkilangi



Uchemshaji wa chumvi kwa njia ya asili.



Msindikaji wa Chumvi akiianika chumvi tayari kwa matumizi.

### **Sekenke**

Eneo hili lipo kijiji cha Nkokilangi, Kata ya Ntwike, Tarafa ya Shelui, ni maarufu kwa machimbo ya madini aina ya dhahabu vile vile kuna pango lililochimbwa na kujengwa reli Kutoka Sekenke hadi Misigiri, shimo hili lilitumiwa na Wakoloni kwa ajili ya kusafirisha madini, hivi sasa limegeuka makazi ya popo ambapo kinyesi chao kimekuwa kikitumiwa na wananchi kama mbolea bora katika kilimo.



Shimo hili lilitumiwa na wajerumani kusafirishia dhahabu kutoka sekenke hadi eneo la Misigiri kwa kutumia kiberenge.

### **Nkonta – Ushora – Ndago**

Kuna mapango ambayo aliishi mtu aliyeitwa Gunda Mpwani alikuwa na nguvu za pekee. Pia eneo hilo lina mwamba wenye nyayo za binadamu za wanyama.

### **Kimagwe**

Eneo hili lipo kijiji cha Ruruma, Kata ya Kiomboi, Tarafa ya Kisiriri, Hapo kuna nyayo za binadamu na wanyama kama vile mbwa, mbuzi na ng'ombe. Nyayo za binadamu huyo zinajulikana kwa jina la Ntigazi (Mugulu wake Ntegazi).



Nyayo za binadamu wa kale maarufu kwa jina la Ntegazi ipo kijiji cha Ruruma-kimagwe.

### **Kisiriri Ikulu ya Mtemi**

Eneo hili lipo kijiji cha Kisiriri Kata ya Kisiriri Tarafa ya Kisiriri, ndipo makazi ya Mtemi wa wanyiramba (Ikulu ya Mtemi). Wananchi wa Wilaya ya Iramba walikuwa wakikusanyika hapo kwaajili ya matambiko mbalimbali kama vile kuomba mvua, kufukuza balaa, mikosi na laana.



Nyumba ya mtemi wa wanyiramba ipo katika kijiji cha kisiriri Iramba.

Watemi wakinyiramba walioiongoza Iramba ni hawawafuatao;

Makala,Kitandu,Shanyaaga,Jwagu,Masesa,Simbo,Mpazi,Kimale,Gelege,Shila,Magile,Kingu,Kingu II,Maziila(Selemani),Gelege II,Selemani I1 na Luther Gelege (Alifariki mwaka 2001).

## **Kyaga**

Eneo hili lipo kijiji cha Kinalilya, Kata ya Kisiriri, Tarafa ya Kisiriri Kuna michoro ya Wanyama kama vile sungura, twiga nk kwenye miamba ya mawe ya Kyaga.



Picha ya mnyama (twiga) iliyochorwa kwenye mwamba - Kinalilya

## **Utamaduni**

Utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine . Utamaduni ndicho kitambulisho kikuu cha taifa na ni kielelezo cha utashi na uhai wa watu wake.Umoja, utulivu na mshikamano ambavyo watanzania tunajivunia vinatokana na utamaduni tuliojijengea.Nguzo za utamaduni ni pamoja na mila na desturi, lugha, sanaa, michezo na historia yetu .

## **Mila na Desturi**

Mila na desturi ni nguzo muhimu sana katika utamaduni wa jamii ye yeyote ile mila huwakilisha matendo na taratibu za jamii. Mila ni sawa na sheria zisizoandikwa. Desturi huelezea namna jamii inavyoendesha mambo yake mila na desturi hujengwa, hukomaa, hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na pia hufifia na hatimaye kupotea.

Desturi huanza kama tabia ya mtu au kundi la watu. Tabia hii ikienea kwa jamii nzima hugeuka kuwa desturi. Desturi zikiota mzizi zikawa ndizo mila namna halali ya kufanya mambo hugeuka kuwa mila. Jamii hukemea tabia mbaya ili zisisambae na kugeuka kuwa desturi. Kwa mfano Wanyiramba wanachukia sana vitendo viovu kama vile matumizi ya madawa ya kulevyta, ubakaji, ulevi, uvivu, uzembe, uzururaji, umalaya, ubaguzi na udhalilishaji wa kijinsia mfano ukeketaji watoto wa kike . Mila na desturi nzuri ni utunzaji wa mali na rasilimali, kuheshimu utu wa watu, tabia ya usafi, uhifadhi na matumizi bora ya rasilimali na mazingira .

## **Utani Bainya Koo na Koo, Wanyiramba na makabila mengine**

Kila ukoo katika kabile la wanyiramba wanao watani wao, kwa kinyiramba huitwa *anishoi kuna* makundi mawili ya watani katika kabile la wanyiramba kama ifuatavyo; Analelya watani wake ni; anakumi, ananangu/anamilambo, anankamba, anankale, anambeu, ananzo-ka, anamwendo na aniyuga.

Watani wa anambua ni kama ifuatavyo; anishungu, anikyili, anishanga, anambala, anangili, anampanda na Anankumbi.

Kwa upande wa makabila mengine, wanyiramba watani Wao Wa asili ni watu wa musoma yaani *wakurya* na *wajita*, watani wengine ni jirani zao *wanyaturu*. Utani wao haukuja hivihivi bali ultokana na matukio mbalimbali katika maisha yao.

### **Ndoa**

Mtoto wa kiume alipofikia muda wa kuoa, aliomba ridhaa toka kwa wazazi wake, nao wazazi wakisharidhia ombi la mtoto wao walitoa ruksa ama Kumchagulia mke mwenye sifa ya uchapa kazi, msafi, mkarimu, mpenda ndugu wa pande zote, nyumbani kwao wasiwe washirikina, maradhi ya ukoma, kifafa na kichaa. Mahari ilitolewa mbuzi 12 na ngombe mmoja, Mama mzaa binti alipewa mbuzi mmoja (mkoaa) kutoka familia ya mtoto wa kiume. Naye mtoto wa kiume alipewa mbuzi mmoja na baba yake kama zawadi. Kabla ya harusi binti aliyelewa anaolewa alikalishwa sehemu maalum na bibi zao kwa lengo la kumfunda ili aweze kuhimili maisha ya

Ndoa halikadhalika kwa kijana aliyetarajia kuoa alipatiwa mafunzo toka Kwa wazee (mababu). Siku ya harusi watu waliandaliwa vyakula mbalimbali kama vile: ugali, kande, nyama ya ngombe, mbuzi na vinywaji kama: Togwa (magae ya nkaata) na pombe (magae ya ntulu), sherehe hizo Zilikua zinaambatana michezo na burudani mbalimbali mfano “ngoma ya winga”.

## **Vyakula**

Wanyiramba wanavyo vyakula vya asili ambavyo huvitumia, vyakula hivyo ni:ugali wa mtama, uwele na mahindi, mboga ni *kyuluga* (mlenda), *nsonga*, *Ndalu* (mlenda) uliokaushwa na kusagwa), *Nsansa* (Majani ya kunde yaliyo pikwa na kukaushwa), akwepa, kukulu, kyumbo nk. vyakula vingine ni indoolo(viazi) na mihogo. Aidha kuna matunda ya asili nayo ni; matogo, nsisai, mbilo, nsingila, mapama, ntundua, mbula, ntunguza, numpilo, nsansampeke, mpumambuli, maungo, mpulu, mbwembwe nk.

Kwa upande wa mavazi Wanyiramba walitumia sana kaniki na lubega ingawa kwa siku hizi mavazi haya, hayavaliwi kutokana na utandawazi. Vazi la kaniki na lubega kwa sehemu kubwa huvaliwa wakati wa matambiko, sanaa na burudani.

Wanyiramba ni wasanii wazuri katika masuala ya sanaa hususani: ufinyanzi, ususi, uchoraji, uchongaji, ngoma, nyimbo nk.

Vile vile Wanyiramba hawapo nyuma katika masuala ya michezo ya jadi kama vile bao, kulenga shabaha, kufukuza kuku, mieleka nk.

Wanyiramba hujiburudisha kupitia burudani mbalimbali kama ngoma ya mbetu, ngoma ya Winga ambayo huchezwa kwenye harusi, mpembe ambayo huchezwa wakati wa mavuno, mara nyingi burudani hizi huambatana na vinywaji kama vile: magae mantulu (pombe iliyotengenezwa kwa mtama) na magae ya nkataa (togwa).


Kadri muda unavyozidi kwenda mbele, Utamaduni wa Wanyiramba unapungua kidogo kidogo. Hivyo zinatakiwa hatua za maksudi kulinda Mila na desturi.

Hakuna kumbukumbu za kutosha zinazoelezea Utamaduni, Mila na desturi, Rasilima na Utalii wa Wanyiramba na kama zipo hazijatunzwa mahali stahili au eneo muhimu.

Baadhi ya Wazee wenyе historia ya Jamii ya wanyiramba wamehifadhi kumbukumbu Vichwani mwao na wala si kwenye maandishi, kwa mantiki hiyo mtu huyu akifariki ndio mwisho wa historia.

Baadhi ya taarifa za Iramba zinazohusu Utamaduni, Mila na Desturi, Rasilimali na utalii zimeandikwa na Wazungu ambapo kwa sehemu kubwa walijikita zaidi kuelezea masuala ya dini na kiasi kidogo sana Utamaduni, Mila na Desturi wa Iramba.





Wananchi wa kijiji cha mingela (Isui) wakijiburudisha kwa ngoma ya jadi Maarufu “mbutu”.

Zamani ngoma ya mbetu ilitumiwa kuwaliwaza wafiwa hususani waliofiwa na wazee vikongwe sio watoto wala vijana. Siku hizi imekuwa iki Tumiwa kama burudani baada ya kazi.

## SURA YA SABA

### **Tarafa, Kata na Vijiji vya Wilaya ya Iramba**

Kwa mujibu wa idara ya mipango, takwimu na Ufuatiliaji wilaya ya Iramba, hadi mwaka 2015 Wilaya ya iramba ilikuwa na **Tarafa nne (4)** Kata **Ishirini (20)** na **Vijiji sabini (70)**, na **Vitongoji 392**. Kwa ufanuzi zaidi tazama jedwali lifuatao hapa chini ambali linaonesha Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji Wilayani Iramba. **Kata** zilizo ongezeko ni mukulu na Old kiomboi na Maluga.

	<b>TARAF</b>		<b>KATA</b>		<b>KLJIJI</b>		<b>KITONGOJI</b>
1	<b>Kinampanda</b>	1	Kinampanda	1	Kyalosangi	1	Ndorobo
						2	Mgogo
						3	Mlekela
						4	Kyalosangi
						5	Mwambao
						6	Kitusha
			2	Uwanza		7	Mtumbili
						8	Mzuu
						9	Mkonkotena
						10	Itinku
						11	Uwanza
						12	Monele
			3	Galangala		13	Munkonze
						14	Galangala
						15	Mugembe
			4	Kisharita		16	Kyulusi
						17	Masangia
						18	Masea
						19	Mgumo
		2	Maluga	5	Ng'anguli	20	Ikyeto
						21	Ng'anguli
						22	Masunkune
			6	Maluga		23	Mitunduruni
						24	Nkulusi
						25	Mighanga
						26	Mitulu
						27	Masngya
						28	Kona
		3	Ulemo	7	Ulemo	29	Madukani

	TARAFA	KATA	KLJIJI		KITONGOJI		
				30	Mpuli		
				31	Majengo		
				32	Msisi		
		8	Kitukutu	33	Kidosa		
				34	Miula		
				35	Kisingu		
				36	Kiele		
				37	Tyengemala		
		9	Misigiri	38	Njiapanda		
				39	Miembeni		
				40	Msimbazi		
				41	Nkingi		
				42	Kichangani		
				43	Kizaga		
	4	Mukulu	10	Mukulu	44	Mkulu A	
					45	Mkulu B	
					46	Mkuu C	
					47	Mkulu D	
			11	Motomoto	48	Stephano Shila	
					49	Mwampiti	
					50	Mtandao	
			12	Simbalungwala	51	Magugu	
					52	Kilambazi	
					53	Shuleni	
					54	Ulongo	
	5	Kyengege	13	Kyengege	55	Ndua	
					56	Mgalilwa	
					57	Magali	
					58	Jengelangulu	
			14	Mugundu	59	Tyandu	
					60	Lyungilo	
					61	Sokoine	
			15	Makunda	62	Monele A	
					63	Monele B	
					64	Ulyang'ombe	
					65	Itunda	
2	Ndago	6	Kaselya	16	Kaselya	66	Msemembo
						67	Mnadani
						68	Madukani
						69	Zanzibar
						70	Mpambaa
						71	Msisi
						72	Izengelangulu
			17	Nsonga	73	Kipimbi	

TARAFA	KATA	KLJIJI	KITONGOJI
		74	Mikoroshoni
		75	Imalamakuo
		76	Mwembeni A
		77	Kati
	18	Mugungia	Ugali
		78	
		79	Msisi
		80	Ndala kati
		81	Mwandu
		82	Ndala juu
7	Ndulungu	19	Mwandoigembe
		83	Nyerere
		84	Rudisha
		85	Shemwela
		86	Kipampa
		87	Igona
		20	Ndulungu
		88	Mjenga
		89	Mkonze
		90	Shemwela
		91	Misughaa
		92	Isuntiya
	21	Mahola	Mahola
		93	
		94	Kipembawe
		95	Ndulungu
	22	Kipuma	Kipuma
		96	
		97	Makungu
		98	Luzilukulu
		99	Fundi majamvi
8	Mtekente	23	Lunsanga
		100	Mtakuja
		101	Kagera
		102	Shuleni
		103	Mnadani
		104	Kigulunsungi
		105	Lunsanga
		106	Kimbai A
		107	Kimbai B
		108	Kimbai C
	24	Msansao	Us wahilini
		109	
		110	Shuleni
		111	Nkalemui
		112	Magoba
		113	Numbanumba
		114	Msansao
		115	Matinje A
		116	Matinje B
	25	Ujungu	Ujungu A
		117	

	TARAFA	KATA	KLJIJI		KITONGOJI
				118	Ujungu B
				119	Ujungu C
				120	Ujungu D
		26 Kisonga		121	Msikitini
				122	Shuleni
				123	Kanisani
				124	Zaire
9	Urughu	27 Urughu		125	Urughu
				126	Msumbiji
				127	Haila
				128	Semu
				129	Sulungai
		28 Mang'ole		130	Mang'ole
				131	Mbuyuni
				132	Mpugizi
				133	Unambiu
		29 Mlandala		134	Usasi
				135	Msombi
				136	Madalawa
				137	Iluwilo
		30 Masimba		138	Mayanzani
				139	Masimba "A"
				140	Masimba "B"
				141	Makio
				142	Utalula
10	Mbelekeses	31 Misuna		143	Madukani
				144	Mpambaa
				145	Mtakuja
				146	Kilambazi
				147	Masunkune
				148	Isenenkwa
		32 Kikonge		149	Mabanda
				150	Nkulusi
				151	Mwasintao
				152	Iloelya
				153	Mpambaa
				154	Mtakuja
				155	Mumuno "A"
				156	Mumuno "B"
				157	Igora
		33 Mbelekeses		158	Mbelekeses
				159	C.C.M
				160	Mpambaa
				161	Mpuli

	<b>TARAFA</b>		<b>KATA</b>		<b>KLJIJI</b>		<b>KITONGOJI</b>
					162		Mbuyuni
			34	Usure	163		Muongano
					164		Azimio
					165		Mapinduzi
					166		Malango
					167		Mpuli B
	11	Ndago	35	Nguvumali	168		Ilongero
					169		Nkulusi
					170		Masimba
					171		Ndago Kati
			36	Mdonkolo	172		Mdonkolo
					173		Kinambua
					174		Igila
					175		Utinde
			37	Zinziligi	176		Kinishanga
					177		Zinziligi
					178		Maluja
					179		Mtakuja
					180		Lunua
			38	Songambele	181		Lyowela
					182		Kibaya Magharibi
					183		Kibaya Mashariki
					184		Jengelangulu
					185		Ushora Kati
					186		Mapera B
					187		Shemwela
			39	Luzilukulu	188		Mapera "A"
					189		Luzilukulu Nga'ambo
					190		Luzilukulu Bondeni
					191		Kabutwa
3	<b>Shelui</b>	12	Shelui	40	Nselembwe	192	Nselembwe
					193		Pangani
					194		Kintende
					195		Sawasawa
					196		Makiki
					197		Tyuta
					198		Ishanga
					199		Nkyala
			41	Nkyala	200		Nkyala
					201		Msansao
					202		Kishomali
			42	Wembere	203		Kinankumbi
					204		Msinsi
					205		Kidui

TARAFA	KATA	KLJIJI	KITONGOJI
		206	Busulwankoko
	43	Tintigulu	207 Kiselelo
			208 Tintigulu
			209 Mlumbi
			210 Bati
	44	Kibigiri	211 Shuleni
			212 Mbuyuni
			213 Mkajuni
			214 Mkuyuni
<b>13</b>	Mgongo	45 Mgongo	215 Mntamba
			216 Mtamba B
			217 Matongo
			218 Majengo
	46	Kizonzo	219 Kizonzo Shule
			220 Kizonzo kati
			221 Bwawani
	47	Mseko	222 Mwamlula
			223 Mseko A
			224 Mseko B
			225 Malendi
	48	Kisonga	226 Kisonga
			227 Laida
			228 Isuna A
			229 Isuna B
<b>14</b>	Mtoa	49 Mgela	230 Stoo
			231 Mgela Kati
			232 Kisua
	50	Mtoa	233 Ibambasi
			234 Mtoa Kati
			235 Mpambaa
	51	Msai	236 Ntimbwe
			237 Dodoma
			238 Lutamula
			239 Msai Magharibi
			240 Msai Kati
			241 Mpambaa
	52	Tyeme	242 Mlungu
			243 Tyeme Mashariki
			244 Tyeme Kati
			245 Katembo
			246 Ikaranga
			247 Mkima
			248 Nkyala
	53	Masagi	249 Masagi Shuleni

	<b>TARAFA</b>		<b>KATA</b>		<b>KLJIJI</b>		<b>KITONGOJI</b>
						250	Kipeke
						251	Mgunga
			54	Kinkungu	252	Stoo	
					253	Miembeni	
					254	Mashineni	
	<b>15</b>	Ntwike	55	Mingela	255	Jengelyampandi	
					256	Mingela	
					257	Tyelu	
					258	Milambo	
					259	Inolelo	
					260	Wagamoyo	
		56	Nsunsu		261	Yulyamwana	
					262	Mongo	
					263	Mnembule	
					264	Nsunsu A	
					265	Nsunsu B	
					266	Juju	
					267	Ng'unga	
					268	Sangasa	
		57	Ntwike		269	Monele	
					270	Munsunsu	
					271	Kisuamando	
					272	Ityanga	
					273	Ityepu	
					274	Msanga	
		58	Nkonkilangi		275	Mnsele	
					276	Nkonkilangi Kati	
					277	Ipuli	
					278	Kisiwani	
					279	Kityugulu	
					280	Kibululu	
		59	Shelui II		281	Miembeni	
					282	Msisi	
					283	Kyulungu	
					284	Ilyomo	
					285	Shelui	
					286	Shungilo	
4	<b>Kisiriri</b>	16	Kisiriri	60	Kisana	287	Kisalulalu
						288	Kilambazi
						289	Kyongolo
						290	Wangu
						291	Nzuwa
						292	Kisana Juu
						293	Kinakumi

TARAFA	KATA	KLJIJI	KITONGOJI
		294	Mpazu
		295	Kintamba
	61	Kisimba	Kisimba
		297	Kimpunda
		298	Igugulya
	62	Kisiriri	Igange
		300	Ntulu
		301	Mazuta
		302	Nsungui
		303	Mugwe "A"
		304	Mugwe "B"
		305	Mgongo
	63	Kinalilya	Diyanange
		307	Shigani
		308	Gulumba
		309	Mlindo
17	Tulya	64	Tulya
		310	Tulya
		311	Mnsele
		312	Bambalaga
		313	Yombo
	65	Migilango	Maugulu
		315	Migilango
		316	Milai
		317	Shauritanga
	66	Doromoni	Doromoni
		318	Doromoni
		319	Kiteka
		320	Geta
		321	Kibigiri
18	Kidaru	67	Luono
		322	Luono
		323	Mdama
		324	Kigaa
		325	Mbuga ya mpoku
		326	Mwamapuli
	68	Tyegero	Samora
		327	Samora
		328	Amani
		329	Nkhuruma A
		330	Nkhuruma B
	69	Kidaru	Mwando
		331	Dukusilu
		332	Mlumba
		333	Twelambwa
		335	Laini
		336	Magema
	70	Ndurumo	Ndurumo
		337	Ndurumo

TARAFA	KATA	KLJIJI	KITONGOJI
		338	Makimamabi
		339	Makale
<b>Mamlaka ya Mji Mdogo Kiomboi</b>			
	19	Kiomboi	340 Lulumba
			341 Shuleni
			342 Zahanati
			343 Soweto
			344 Inala 'A'
			345 Kizega
			346 Mdunku
			347 Igumo
			348 Ng'una
			349 Lunsanga
			350 Mgalamo
			351 Kyambi
			352 Inala 'B'
			353 Tutu "A"
			354 Tutu "B"
			355 Mlutani
			356 Mguluka
			357 Like
			358 Msisi
			359 Kikaku
			360 Nkananga
			361 Mguluko
			362 Kilundo
			363 Shati kati
			364 Shengelo
			365 Lowa A
			366 Lowa B
	20	Old-Kiomboi	367 Madukani
			368 Kyaya
			369 Mampampa
			370 Yombwe
			371 Mang'ata
			372 Pyululu
			373 Magula
			374 Meli Kati
			375 Mgagai
			376 Melinsele
			377 Mbutia
			378 Ntalange
			379 Nhuile
			380 Tigwambuli

TARAFA	KATA	KLJIJI	KITONGOJI
		381	Tinku
		382	King'inga
		383	Msoma
		384	Msinsi
		385	Mlangali
		386	Miembeni
		387	Kibaoni
		388	Idemu
		389	Zumagi
		390	Mlingoti
		391	Mlumbita
		392	Mluluma
4	20	70	392

Hivi sasa wilaya ya Iramba chini ya mkuu wa wilaya Emmanuel Luhahula ina mpango mkakati wa kufufua kilimo cha pamba na kuanzisha zao la korosho ambapo yataongeza idadi ya mazao ya biashara ukijumuisha na zao la alizeti.

Uzalishaji wa mazao haya ukitokea kwa kiwango cha juu, itabadilisha kabisa hali ya maisha ya wananchi wa Iramba kutoka maisha duni na kuwa bora kwani itaongeza pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Aidha sera ya serikali ya uchumi wa viwanda na ajira kwa vijana itakuwa imetekelzeza vema ili kufikia Uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025.

**'MUNGU IBARIKI IRAMBA NA WATU WAKE, MUNGU  
IBARIKI TANZANIA'**